

MKATABA WA UPANGISHAJI

MKATABA huu wa upangishaji umefanywa hapa DODOMA leo hii tarehe 01/02/2023 Mwezi 02.....2023.

KATI YA

M/S THAKER SINGH wa S.L.P 62, Dodoma ambaye katika mkataba huu ataitwa "MWENYE ENEO" kwa upande mmoja,

NA

JOSEPH BERNADO SIMKOKO wa S.L.P 4169, Dodoma ambaye katika mkataba huu ataitwa "MPANGAJI" kwa upande wa pili.

KWA KUWA mwenye eneo anamiliki kihalali nyumba iliyopo eneo la Area D Mtaa wa Kemi, ndani ya Jiji la DODOMA na ana nia thabiti ya kumpangisha mpangaji eneo la wazi lililopo katika nyumba hiyo,

NA KWA KUWA mpangaji baada ya kuona eneo hilo na kuridhika nalo amehiyari kupanga eneo hilo kwa masharti yafuatayo hapa chini:

HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA YAFUATAYO:

1. Kodi ya pango itakuwa **Sh. 600,000/=** (Shilingi Laki Sita) tu kwa mwezi sawa na **Sh. 36,000,000/=** (Shilingi Milioni Thelathini na Sita) tu kwa miaka mitano(5).
2. Mkataba huu utadumu kwa muda wa miaka mitano (5) kuanzia tarehe **01/02/2023** mpaka tarehe **01/02/2028** isipokuwa tu muda wa mkataba unaweza kuongezwa endapo pande zote mbili zitaridhia kufanya hivyo.
3. Endapo muda wa mkataba utafikia ukomo na pande zote zikakubaliana kuongeza muda wa mkataba, masharti ya mkataba yanaweza kubadilishwa au yakabaki vile vile kutegemeana na pande zote zitakavyokubaliana isipokuwa tu upande wa wenye nia ya kuongeza muda wa mkataba utatakiwa kutoa taarifa ya maandishi kwa upande mwingine kueleza nia hiyo angalau siku tisini kabla ya muda wa mkataba huu kuisha na taarifa hiyo itatakiwa kujibiwa ndani ya siku kumi na nne tangu siku ilipopokelewa.

4. Taarifa ya kuongeza muda wa mkataba au majibu ya taarifa hiyo vitawasilishwa kwa kukabidhi kwa mkono kwenye eneo la kawaida la biashara au nyumbani kwa mtu anayepelekewa taarifa au majibu ya taarifa hiyo.
5. kwa mpangaji wala kufidiwa kwa namna yoyote ile kwake na Jengo au majengo husika yaliyojengwa na Mpangaji katika eneo la Mwenye eneo yatakuwa ni mali ya mwenye eneo na yatabaki chini yake bila mpangaji kufanya uharibifu wa namna yoyote ile kwa maksudi katika jengo au majengo hayo wakati wa kuondoka.
6. Mpangaji amekwisha kabidhiwa eneo husika kabla ya kusaini Mkataba huu.
7. Mpangaji atatumia eneo hilo kwa matumizi ya **BIASHARA TU**.
8. Mpangaji kwa makubaliano na mwenye eneo wamekubaliana kama ifuatavyo.
 - (a) Mpangaji atawajibika kutunza majengo/ jengo alilojenga, eneo husika na mazingira yake katika hali ya usafi kwa mujibu wa kanuni za afya za Jiji na za Nchi.
 - (b) Kutompangisha au kugawa jengo alilojenga au eneo husika kwa mtu mwingine yeyote bila ya ruhusa ya mwenye eneo kimaandishi.
 - (c) Kumruhusu mwenye eneo au mwakilishi wake kuingia katika eneo husika wakati wowote ule mchana kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa mazingira yake.
 - (d) Mwisho wa Mkataba huu, kukabidhi majengo/ jengo alilojenga na eneo husika kwa mwenye eneo vyote vikiwa katika hali nzuri.
 - (e) Mpangaji atapaswa kulipa ankara ya umeme na maji kwa muda wote wa mkataba kadri anavyotumia
9. Mwenye eneo anaahidi yafuatayo;
 - (i) Iwapo mpangaji atatimiza masharti mengine yote yaliyoanishwa ndani ya Mkataba huu, basi mwenye eneo au Mrithi au Mwakilishi wake

atamwacha mpangaji huyo atumie eneo hilo kwa AMANI bila bugudha yoyote.

(ii) Mkataba huu unaweza kuvunjwa kwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja ki-maandishi ya kusudio la kufanya hivyo.

(iii) Mwenye eneo atawajibika kulipa kodi zote za Kiwanja na majengo kama inavyoainishwa na Mamlaka husika.

KWA KUSHUHUDIA YALIYOANDIKWA HUMU PANDE ZOTE MBILI ZIMEWEKA SAINI ZAO KAMA IFUATAVYO KWA TAREHE MWEZI NA MWAKA KAMA ILIVYOONYESHWA HAPA CHINI.

UMESAINIWA na KUWASILISHWA na
ambaye M/S THAKER
SINGH
namfahamu binafsi/ametambulishwa
naleo tarehe..... mwezi..... 2023

SAINI:
JINA : Balwinder Singh Uesri
ANUANI: Po. Box 62 Dodoma
CHEO: Director

MBELE YA:
SAINI:
SANDUKU LA POSTA: 4169
DODOMA

WADHIFA: WAKILI

UMESAINIWA na KUWASILISHWA na
ambaye JOSEPH BERNADO
SIMKOKO
namfahamu binafsi/ametambulishwa
naleo tarehe
..... mwezi2023


.....
MWENYE NYUMBA




.....
MPANGAJI

MBELE YA:

SAINI:

SANDUKU LA POSTA: 4169

DODOMA

WADHIFA: WAKILI

